Kukamatwa kwa watu hao ni matokeo ya kura za siri zilizopigwa na wananchi wa maeneo hayo kuwataja wanaohusika na ziara ya hivi mkoani Simiyu ya Mkuu wa Jeshi la Polisi Inspekta Jenerali (IGP), Simon Sirro aliyetangaza oparesheni ya siku 10 ya kuwanasa watuhumiwa wa mauaji hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari Lamadi juzi, kiongozi wa operesheni hiyo ya polisi, Salum Hamdun alisema watuhumiwa hao wamekamat-

wa karatasi maalum aliorianywa kwa siku tatu.

"Miongoni mwa wanaoshikiliwa wamo waganga wa kienyeji na wapiga ramli chonganishi," alisema Hamdun.

Februari 14 mwaka huu wakazi wa Lamadi walipiga kura za siri zilizosimamiwa na mkuu wa wilaya ya Busega, Tano Mwena kuwabaini wanaohisiwa kuhusika na matukio ya mauaji ya watoto wa kike yanayotikisa eneo hilo tangu mwishoni mwa mwaka jana.

Kabla ya tukio la kupiga kura,

Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Uhamiaji na Polisi ambao hata hivyo baadhi yao wamenyooshewa vidole na wananchi kuwa wanahusika kwa kuwaachia watuhumiwa wanaokamatwa kuhusiana na mauaji hayo bila kuwafikisha mahakamani.

Katika siku za hivi karibuni matukio ya mauaji hasa ya watoto wadogo wa kike yamekuwa yakitikisa mji wa Lamadi na kuibua hofu kubwa miongoni mwa wananchi.

wengine katika kesi hiyo kuwa ni aliyekuwa kaimu katibu jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori Burunge, Francis Mwasombele na mwenyekiti wa kijiji cha Vilima Vitatu, Erasto Belela Kou.

Amesema washtakiwa hao wameshtakiwa kwa kosa la kukwepa kodi kinyume na sheria ya magari (ushuru wa usajili namba 124/2006) kifungu cha 15 (b).

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 4 mwaka huu.

**(Joseph Lyimo)**

Iringa kutoka Benki ya CRDB vyenye thamani ya Sh60 milioni.

Hapi alisema Serikali imetenga bajeti kwa ajili ya elimu bure na wadau wanajitoa kuboresha elimu hiyo.

"Wapo waliokataliwa kusoma kwa kukosa ada, inawezekana wengine wanataka kusoma lakini wazazi wao wanawapeleka kufanya kazi za ndani, kulima au pengine hawataki bila sababu, mie siamini kama mtoto aliyesoma na akafaulu akatae kuendelea na shule bila sababu, hivyo tutahakikisha tunawakamata wazazi wote hata kama watakuwa 20,000 ili waeleze walipo watoto hawa na kwanini hawajaripoti shule mpaka leo," alisema.

Hapi aliliagiza jeshi la polisi kuwasaka wazazi wote walioshindwa kuwapeleka shule watoto wao waliofaulu na badala yake kuwasafirisha kwenda kufanya kazi za ndani.

Kwa upande wake, mkurugenzi mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema Serikali imejikita kutoa elimu bure hivyo wao kama wadau wanajitokeza kuwapa wanafunzi mazingira bora ya kusomea.

Naye mwakilishi wa mwenyekiti wa bodi ya CRDB, Neema Mori alitoa rai kwa wanafunzi kuwa na nidhamu

## MSAMAHA

Mkazi wa kijiji cha Lola wilayani Chunya, Subira Lugegeta akiwa amepiga magoti mbele ya mkuu wa mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila ili kumuombea msamaha mume wake baada ya mkuu huyo wa mkoa kuamuru kukamatwa na kuwekwa mahabusu pamoja na wenzake watatu kwa tuhuma za kuchochea migogoro na kuwachonganisha viongozi wa Serikali ya kijiji na wananchi kijijini hapo. **Picha na Godfrey Kahango**



## Faini za uvuvi haramu kujenga madarasa

**Ukerewe.** Mkuu wa wilaya ya Ukerewe, Cornel Magembe amesema wilaya hiyo imeanza kukusanya zaidi ya Sh700 milioni za kukamilisha ujenzi wa vyumba 316 vya madarasa vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi ili kukabiliana na msongamano wa wanafunzi darasani.

Amesema moja ya mikakati yao ni kufanya operesheni dhidi ya uvuvi haramu na fedha zitakazopatikana kutokana na faini zitaboresha shule za msingi na sekondari na kwamba wameshafanikiwa kupata zaidi ya Sh100 milioni.

Ofisa elimu ya msingi halmshauri hiyo, Imelda Lubengo amesema wanafunzi wamepangwa kwa uwiano wa 76 kwa darasa badala ya 45 kama ilivyo kwenye sera ya elimu

## 60mil

**Thamani ya madawati na madarasa mawili yaliyojengwa na CRDB.**